

**MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI CHA TAREHE 19/01/2022
KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA MAGU**

WAJUMBE WALIOHUDHURIA:

- | | | |
|--------------------------|---|-------------|
| 1. Wilbard Bandola | - | Mwenyekiti |
| 2. Peter M. Manoko | - | Katibu |
| 3. Masunga Mwagala | - | Mjumbe |
| 4. Amandus Mboya | - | Mjumbe |
| 5. Adolph Ritte | - | Mjumbe |
| 6. Adv. Merchades Rusasa | - | Mwanasheria |

SEKRETARIETI:

- | | | |
|------------------------|---|-----|
| 1. Erasmus K. Katabazi | - | PMU |
| 2. Maigu Gisema | - | PMU |
| 3. Mary William | - | PMU |

AGENDA ZA KIKAO:

1. Kufungua Kikao.
2. Kusoma na kuthibitisha agenda
3. Kupitia na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha tarehe 15/12/2021
4. Kupitisha njia ya ununuzi kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya watumishi (3 in 1 katika Hospitali ya Wilaya ya Magu kupitia fedha za mradi wa UVIKO-19 (TCRP)
5. Mengineyo.
6. Kufunga kikao.

MUHT NA. 06/2021-2022/AGENDA NA. 1: KUFUNGUA KIKAO.

Mwenyekiti alifungua kikao hapo saa 4:05 Asubuhi kwa kuwakaribisha wajumbe wote ili waweze kushiriki na kutoa michango yao katika agenda zote zilizopo mezani.

MUHT NA. 06/2021-2022/AGENDA NA. 2: KUSOMA NA KUTHIBITISHA AGENDA

Mwenyekiti alimwomba Katibu asome agenda zilizopo katika mwaliko wa kikao cha bodi ya zabuni. Katibu alisoma agenda zote, ambapo wajumbe wote walipitia na kuthibitisha agenda sita (6) zilizopo mezani na kuliridhia kuwa agenda zote zijadiliwe.

MUHT NA. 06/2021-2022/AGENDA NA. 3: KUPITIA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 15/12/2021

Mwenyekiti aliwaongoza wajumbe kupitia muhtasari wa kikao kilichopita cha tarehe 15/12/2021 kwa kupitia agenda zote zilizojadiliwa na wajumbe ukurasa kwa ukurasa. Baada ya kupitia wajumbe kwa ujumla wao waliuthibitisha muhtasari huo na ndipo ukasainiwa kuwa kumbukumbu sahihi ya kikao.

MUHT NA. 06/2021-2022/AGENDA NA. 4: KUPITISHA NJIA YA UNUNUZI KWA AJILI YA UJENZI WA NYUMBA YA WATUMISHI (3 IN 1 KATIKA HOSPITALI YA WILAYA YA MAGU KUPITIA FEDHA ZA MRADI WA UVIKO-19 (TCRP))

Katibu wa bodi ya zabuni aliwapitisha wajumbe wa bodi ya zabuni katika agenda hii kwa kuwaeleza kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Magu katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 imepokea kiasi cha Tsh. 90,000,000.00 kupitia mpango maalum wa Ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya UVIKO -19. Aidha katika Halmashauri ilitekeleza maelekezo ya awali ya kutumia taratibu ya za kumpata mkandarasi hata hivyo mpaka siku ya mwisho ya kuwasilisha Kotesheni ni wazabuni watatu tu waliojitokeza na gharama zao zilikuwa juu kuliko kiwango cha bajeti iliyopo ya ujenzi wa Nyumba ya watumishi. Wazabuni waliowasilisha nyaraka za zabuni siku ya ufunguzi ya tarehe 11/01/2022 walikuwa kama ifuatavyo:-

Na.	Wazabuni walioomba	Gharama ya Ujenzi (Pamoja VAT)
1.	Dynamic Experience TZ Limited wa S.L.P. 72876, Dar es Salaam	167,377,867.00
2.	M/S Ilemela Joint Limited wa S.L.P. 1404, Mwanza	194,667,402.50
3.	M/S Koja's Builders & General Supply Ltd wa S.L.P. 11126, Mwanza	165,198,250.00

Baada ya kupitia zabuni hizo na kwa kuzingatia barua ya tarehe 13/01/2022 yako yenye kumb. AH.161/298/01 ya tarehe 03/06/2022 kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - TAMISEMI iliyotoa maelekezo kwa Wakurugenzi ambao walikuwa hawajapata wakandarasi mpaka kufikia tarehe ya barua hiyo ilipotolewa kutumia 'Force Account' kutekeleza miradi hiyo kwa wakati na kwa ubora unaotakiwa

Katika kutekeleza maelekezo hayo, Kitengo cha Menejimenti ya ununuzi (PMU) kilipendekeza kuwa itumike njia ya 'Force Account' katika utekelezaji wa mradi huu badala ya kutangaza kwa awamu nyingine kwa kuwa itaendelea kuchelewesha utekelezaji.

- **Maazimio:** Bodi ya Zabuni imepitisha njia ya 'Force Account' itumike katika ujenzi wa nyumba ya watumishi (3 in 1 katika Hospitali ya Wilaya ya Magu kupitia fedha za mradi wa UVIKO-19 (TCRP):-

MUHT NA. 06/2021-2022/AGENDA NA. 5: MENGINEYO.

Hakukuwa na Mengineyo.

MUHT NA. 06/2021-2022/AGENDA NA. 6: KUFUNGA KIKAO

Mwenyekiti alifunga kikao saa 5:14 asubuhi kwa kuwashukuru wajumbe kwa michango yao ukizingatia kikao kuchukuwa muda mrefu.



MWENYEKITI

UMETHIBITISHWA



KATIBU

TAREHE: 08/02/2022